**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA**
**BODI YA USIMAMIZI WA STAKABADHI ZA GHALA**

# TANGAZO KWA UMMA

Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) ni taasisi chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara iliyoundwa kwa **Sheria ya Stakabadhi za Ghala Sura ya 339 R.E. ya Mwaka 2016**. Bodi imepewa majukumu chini ya Kifungu 5 (a-j) cha Sheria hiyo ikiwemo kutoa leseni kwa Waendesha Ghala, Meneja Dhamana na Wakaguzi wa Ghala.

Bodi inawatangazia wamiliki wa ghala zote wanaotarajia ghala zao kutumika katika biashara ya Stakabadhi za Ghala Msimu wa Mwaka 2024/2025 hususan katika mazao ya ufuta, kakao, korosho na jamii ya kunde kuwa; kwa kuzingatia **Kanuni ya 15(2) na Sehemu B (2) ya Kanuni**; Bodi inatarajia kuanza zoezi la ukaguzi na uhakiki wa hali na miundombinu ya ghala. Hivyo, mnatakiwa kuwasilisha maombi ya ukaguzi ili kushiriki zoezi hilo litakalowezesha kubaini viwango vya ghala hizo kwa mujibu wa Sheria na kutoa mapendekezo ya kuboresha ili kufikia viwango vinavyotakiwa pale inapohitajika.

Zoezi hili linalenga kufanya utambuzi wa ghala zinazofaa na pia kuondoa ghala zisizofaa ili kufanya maandalizi ya misimu mapema na kuepusha usumbufu unaoweza kujitokeza wakati wa msimu unapoanza.

Pamoja na mambo mengine, waombaji wote mnaelekezwa yafuatayo:-

i. Kuwasilisha barua ya maombi ya kufanyiwa ukaguzi;
ii. Kujaza Fomu Maalumu ya Taarifa za Ghala (Imeambatishwa)
iii. Kuwasilisha nakala za nyaraka za umiliki wa ghala; na
iv. Orodha ya mazao yanayotarajiwa kutumika katika ghala hilo.

Ghala zote zitakazokidhi viwango ndizo zitakazotumika na Waendesha Ghala katika msimu mwaka wa 2024/2025

Maombi yote ya ukaguzi yawasilishwe kupitia **info@wrrb.go.tz;** au **kupitia S.L.P. 2095, Dodoma;** au Ofisi za Bodi zilizopo **Block 03/Plot 23** Mtaa wa Nyerere (Karibu na Nyeyere Square) **Jijini Dodoma**.

Imetolewa,

**MKURUGENZI MTENDAJI**

**15 Machi 2024**

# Kiambatisho: Fomu ya Maalum Taarifa za Ghala

| | |
|---|---|
| **Jina la Ghala:** | ………………………………………… |
| **Jina la Mmilki:** | ………………………………………… |
| **Simu:** | ………………………………………… |
| **Barua pepe** | ………………………………………… |
| **Mkoa** | ………………………………………… |
| **Wilaya** | ………………………………………… |
| **Kata** | ………………………………………… |
| **Majira ya Nukta** | ………………………………………… |

| N | Taarifa za Miundombinu | Weka Alama ya (✓) |
|---|---|---|
| 1 | **Aina ya mzani*** | |
| | Mzani wa daraja | |
| | Mzani wa jukwaa | |
| | Mzani mdogo | |
| 2 | **Eneo la upakiaji na ushushaji** | |
| | Eneo maalumu lililoinuka | |
| | Mikanda inayotembea | |
| | Fork lift | |
| 3 | **Mazingira kuzunguka ghala** | |
| | Mifumo ya utiririshaji maji kutoa eneo la ghala | |
| | Mazingira masafi na kuridhisha | |
| | Kutokuwepo kwa vitu/dutu/shughuli hatarishi karibu na ghala | |
| | Vyoo safi na salama | |
| 4 | **Hali ya jengo*** | |
| | Sakafu ya zege | |
| | Sakafu ya sementi | |
| | Sakafu ya udongo | |
| | Bati imara | |
| | Kuta imara | |
| 5 | **Vifaa vya kudhibiti moto*** | |
| | Kasiki inayohimili moto | |
| | Mpira wa maji ya kuzima moto | |
| | Mtungi wa kuzima moto | |
| | Ving'ora vya tahadhari ya moto | |
| | Ndoo za mchanga | |
| 6 | **Mifumo ya maji na nishati** | |
| | Uwepo wa umeme wa TANESCO | |
| | Uwepo wa umeme wa jua | |
| | Uwepo wa umeme wa jenereta | |
| | Maji ya Serikali | |
| | Maji binafsi/kisima | |
| 7 | **Mfumo wa mawasiliano na TEHAMA*** | |
| | Uwepo wa mtandao wa simu | |
| | Sanduku la posta | |
| | Uwepo wa barua pepe/fax | |
| | Uwepo wa mtandao wa intaneti | |
| | Uwepo wa kanzidata | |
| 8 | **Mifumo ya usalama** | |
| | Taa za usalama ghalani | |
| | Ving'ora vya tahadhari ya wezi | |
| | Kamera za usalama | |
| 9 | **Milango ya ghala*** | |
| | Milango ya mbao | |
| | Milango ya chuma | |
| | Milango ya grili | |
| | Milango ya bati | |
| 10 | **Uzio wa ghala** | |
| | Ukuta wa tofali | |
| | Uzio wa nyaya/senyenge | |
| | Uzio wa uoto | |
| 11 | **Uhifadhi sampuli** | |
| | Kasha maalumu la sampuli | |
| | Rafu maalumu ya sampuli | |
| | Chumba maalumu cha sampuli | |
| 12 | **Utiririshaji maji kutoka ghalani** | |
| | Mitaro maalum ya kutoa mazingira ya ghala | |
| | Gutters za kutiririsha maji | |
| | Mwinuko salama usiotuwamisha maji | |
| 13 | **Udhibiti wadudu waharibifu** | |
| | Wavu maalumu kuzuia wadudu | |
| | Vizuizi vya wadudu kuingia ghalani | |
| | Ghala kutokuwa na mianya ya kuingiza wadudu ghalani | |
| 14 | **Mfumo wa upoozaji ghala** | |
| | Dirisha la ghala juu ya sakafu | |
| | Dirisha la ghala juu ya linta | |
| | Milango ya ghala mbele na nyuma | |
| 15 | **Ufikaji ghalani** | |
| | Barabara ya lami | |
| | Barabara ya vumbi | |
| | Barabara ya marram | |
| 16 | **Ofisi ya ghala** | |
| | Nje ya ghala | |
| | Ndani ya ghala | |
| 17 | **Urefu wa msingi** | |
| | Angalau mita 1 kutoka usawa wa chini | |
| | Angalau mita 0.5 kutoka usawa wa chini | |
| 18 | **Ujazo wa ghala*** | |
| | Zaidi ya tani 5000 | |
| | Kati ya 1000 na chini ya 5000 | |
| | Kati ya 200 na chini 1000 | |
| | Chini ya 200 | |
| 19 | **Vifaa vingine vya ghala*** | |
| | Uwepo wa pallets ghala zima | |
| | Uwepo wa kipima unyevu | |
| | Vifaa vya kupima ubora | |
| | Maturubali | |
| | Kompyuta ghalani | |
| 21 | **Vipimo vya Ghala** | |
| | Urefu | |
| | Upana | |
| | Kimo (hadi chini ya venti) | |
| | **Uzito (tani)** | |